

UFUNUO SEHEMU YA 1

Yohana Mt. 14:21, *“Yeye aliye na amri zangu, na kuzishika, yeye ndiye anipendaye; naye anipendaye atapendwa na Baba yangu; nami nitampenda nakujidhihirisha kwake”.*

Sikiliza kile nabii wa Mungu anavyosema juu ya hilo: “Tena umewajaribu wale wajiitao mitume, nao sio, ukawaona kuwa waongo”, (Ufunuo 2:2-3). Jamani, huo ni msemu wa kukata “Umewajaribu wale wajiitao mitume”. Je hilo silo jambo la kijasiri? Watu wana haki gani ya kuwajaribu wale wajiitao mitume? Na wanawajaribu namna gani?

Hii hapa katika Wagalatia 1:8,” Lakini ijapokuwa sisi au mitume au malaika wa mbinguni, atawahubiri ninyi injili yoyote isipokuwa hiyo tuliyo wahubiri, na alaa niwe” Mitume ndio waliowaletwa watu Neno halisi la asili. Neno hilo halisi la asili halingeweza kubadilika, hata nukta au kistari chake. Paulo alijua Mungu ndiye aliyekuwa amenena naye, kwa hiyo akasema, Hata kama mimi nikija na kujaribu kutoa ufunuo wa pili kujaribu kufanya badiliko moja dogo katika yale niliyotoa hapo kwanza, na nilaaniwe”. Unaona, Paulo alijua ufunuo huo wa kwanza, ulikuwa ni sahihi. Mungu hawezi kutoa ufunuo wa kwanza kisha ufunuo wa pili. Kama angalifanya hivyo, Yeye angekuwa anabadili nia yake. Yeye anaweza kutoa ufunuo, kisha auongeze, kama alivyofanya katika Bustani ya Edeni wakati alipomwahidi mwanamke uzao, halafu baadaye akasema huo uzao ulibidi uje kupitia kwa Ibrahimu, na halafu baadaye akasema ungekuja kwa ukoo ule ule katika Daudi. Lakini huo ulikuwa ufunuo ule ule. Uliwapa tu watu habari zaidi kuwasaidia waupokee na kuufahamu.

Lakini Neno la Mungu haliwezi kubadilika. Ule uzao ulikuja tu kama vile ulivyofunuliwa. Haleluya. Hebu basi angalia yale hao mitume wa uongo walivyokuwa wakifanya. Wao walikuja na Neno lao wenyewe. Waefeso wale walilijua hilo Neno kama vile Paulo alivyokuwa amelifundisha. Wao walikuwa wamejaa Roho Mtakatifu kwa kuwekewa mikono na Paulo. Waliwaangalia hao mitume wa uongo machoni na kusema, Ninyi hamsemi yale aliyosema Paulo. Ninyi, basi, ni waongo! Hilo linauwasha moto moyo wangu rudini kwenye Neno!.

Kanisa, pia, limeondoka kwenye kile kitu cha asili lilichokuwa. Limekuwa mbegu iliyochanganyika. Hiyo ni kusema, kanisa la uwongo ni mbegu iliyochanganyika. Watu wanasema, “ mimi ni mbaptisti.” Haikuwa hivyo pale mwanzo. “ mimi ni Mmethodisti”. Haikuwa hivyo tangu mwanzo.

Badala ya Neno la moja kwa moja la Mungu, badala ya watu waliojazwa na Roho katika Kanisa na walio ongozwa na Roho na kupewa ufunuo, sasa kuna maungamo, na sheria za kujitungia, na mahisio ya kielimu ya watu waliosoma. Kusoma kumechukua mahali pa ufunuo. Hoja zimechukua mahali pa imani. Utaratibu umechukua mahali pa sifa za pamoja katika Roho Mtakatifu. Haikuwa hivyo tangu mwanzo. Jamii yote imebadilika Kanisa limekuwa mbegu mchanganyiko. [1]

Sasa, walifanya nini? Hawakulijua hilo. Leo wanadamu wanatembea bila kujua; hawajui kuwa hiyo ni kweli. Wanafikiri ni aina ya uzushi. Hawachimbi chini kiasi cha kuingia katika roho ya ufunuo. Hawaombi vya kutosha; hawamwiti Mungu kiasi cha kutosha. Wanayachukua kiwepesiwepesi, “Oh, vema, Naamini, ni Mungu kweli. Shetani huamini jambo hilo, shetani analiamini hilo zaidi ya watu wengine wanavyodai kuamini. Shetani analiamini hilo na kutetemeka (Yakobo 2:19). Watu wanaliamini hilo na wanaendelea tu, lakini shetani anatetemeka, akijua hukumu yake inakuja. Na watu wanaliamini hilo na hawajali sana, kwamba hukumu inakuja [2].

Yesu aliwauliza Wanafunzi wake wakati mmoja.” Watu wanasema kuwa mimi ni nani? Na wengine walisema, wewe ni Nabii”. Wengine walisema, “ Ni mmoja wa Nabii wa Agano la kale amefufuka”. Na,”wewe u Musa “ au Eliya au kitu Fulani akasema, nimewauliza ninyi, mnasemaje?

Na Petro akasema, Wewe ni Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai” (Matayo 16:13-20).

Akasema, umebarikiwa wewe, Mwana wa Yona. (Simoni, mwana wa Yona), kwa maana mwili na damu havikukufunulia hili. Hukujifunza hilo kutoka kitabuni, au kutoka kwenye kanuni, au kutoka kwenye Katekismo. Baba yangu, aliyeminguni, ndiye aliyekufunulia hili” Hapo sasa unamuona muamini halisi; ufunuo wa kiroho wa Neno. Unaona? Sasa, na juu”Wewe ndiwe Simoni na juu ya Mwamba huu, wa ufunuo wa mimi ni nani, nitalijenga Kanisa langu, na milango ya kuzimu kamwe haitalishinda”. Unaona?

Sio ajabu Simoni alisema”Twende kwa nani?” Yesu aligeuka akasema na “Ninyi mnataka kuondoka?. Nao wakasema Bwana, twende kwa nani na wewe unayo maneno ya uzima? Wewe ni wa pekee. Siyo tu alikuwa na maneno ya uzima, Yeye alikuwa Neno la uzima, Unaona? Alikuwa Neno la uzima. Na Simoni kwa uhakika alilitambua hilo. Na alipolitambua hilo, ndilo lililoshikilia tumaini lake, kwa sababu ilifunuliwa kwake kwamba alikuwa Neno lililo hai (Yohana 6:60-71).

Sasa huyo ni mwaminio halisi wakati Roho mtakatifu, siyo kushawishiwa na mtu Fulani, siyo kwa kitu chochote lakini Roho Mtakatifu anapokufunulia wewe Neno lake, na unaliona Neno limewekwa wazi, limethibitishwa; ndipo Roho wa Mungu anakuja na kuingia katika huo wakati na kuufanya udhihirike [3].

Mara nyingi, Petro alipoita na kusema, wewe ni Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai”. Sasa , angalia, umebarikiwa wewe Simoni Bayona (hilo laamanisha mwana wa Yona) umebarikiwa wewe, kwa maana mwili na damu havikukufunulia hili. (kamwe hukulisoma shuleni). Lakini Baba yangu aliye mbinguni amekufunulia wewe”. Angalia kile alichomo mwambia, Juu ya mwamba huu...” Huyo ni Petro, mbegu ya Mungu iliyochaguliwa kimbele ambayo imepokea Nuru hii na kupewa funguo za ufalme. “Juu ya mwamba huu wa ufunuo wa Yesu ni nani.....” Yeye ni udhihirisho kamili wa Mungu. “juu ya mwamba”..... siyo Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu, na yeye akiwa ni nafsi ya pili..... juu ya mwamba huu nitalijenga kanisa langu, na milango ya kuzimu kamwe haitaweza kulianguka chini – haitaweza kulishinda. Nitalijenga kanisa langu juu ya mwamba huu.” Ufunuo wa Yesu Kristo. Angalia, Kristo ndani yako linamfanya Kristo ndani yako. Inamfanya awe chimbuko la uhai wa ufunuo.Unaona? Maisha ya kristo ndani yako inamfanya awe chimbuko la ufunuo. Kristo katika Biblia iwe ufunuo mkamilifu wa kristo. inakufanya wewe ufunuo mkamilifu wa jambo lote. (Kolosai 1:26-29; 2:1-3) Unaona kile ambacho Mungu anajaribu kukifanya? [4].

Sasa kuna mabishano mbalimbali juu ya hayo. Warumi, wakatoliki husema, yeye alilijenga juu ya Petro, : Mwaona, na kama hiyo ni kweli, Petro alianguka katika aibu (Luka 22:54-62) kwa hiyo haikuwa hivyo. “Hilo, bila shaka halikujengwa juu ya Petro, Petro, jiwe dogo. Halafu tena waprotestant kusema, ya kwamba yeye alilijenga juu yake, Yesu Kristo. Sikusudii kuwa tofauti, bali sikubaliani nao. Yeye hakulijenga kamwe juu ya yeyote kati yao.

Yeye alilijenga juu ya ufunuo wa Yeye ni Nani yeye alisema heri wewe Simoni, Mwana wa Yona, mwili na damu havikukufunulia hili, bali baba yangu aliye mbinguni amekufunulia hili’ si kwa maarifa! Hukujifunza haya katika vitabu. Hukujifunza kwa kujiunga na Kanisa. Hukujifunza haya madukani. Hukujifunza! Bali kwa Roho Mtakatifu mwenyewe ameuleta utu wa Yesu Kristo kwako. Basi, juu ya Mwamba huu nitalijenga kanisa langu, na milango ya kuzimu haitalishinda”. Hiyo kiu takatifu imetulizwa katika utu wa Yesu Kristo. Hivyo ndivyo. Hicho ndicho kitu tunachotaka kutafuta, kutuliza hiyo kiu kwa hicho. Sawa tunaona ya kwamba hatuna budi. [5].

Ni nini kuzaliwa mara ya pili? Unasema,”vema, ndugu Branham, Ni nini kuzaliwa mara ya pili? Ni ufunuo wa binafsi wa Yesu Kristo kwako. Amen! Unaona? Siyo umejiunga na kanisa, umepeana mikono; umefanya kitu Fulani cha tofauti ; umeseme kanuni; umeahidi kuishi kwa kanuni za sheria; lakini Kristo,

Biblia... Yeye ni Neno lililofunuliwa kwako na haijalishi mtu atasemaje, au kutatokea nini ni Kristo, mchungaji, kuhani, yeyote iwayo..... Ni kristo ndani yako. Huo ni ufunuo ambao kanisa limejengwa juu yake.

Unasema, “Vema, mimi ni mluteri”, “mimi ni mbaptist”,”mimi ni mpresbyteria”. Hilo halimaanishi kitu kwa Mungu, siyo chochote, siyo kupiga vidole vyako. Ni nini? Ni Kristo anapofunuliwa, na yeye ni neno. Na wakati Neno linapofunuliwa, linajieleleza lenyewe. Unaona? Hilo ni kusudi la Mungu kwa Yesu Kristo, kujifunua mwenyewe, kuchukua sheria zake mwenyewe na kuishi kwa sheria zake, na kutimiza sheria zake kwa kifo (Rumi 8:1-4). Kristo, Mungu alikufa katika mwili ili kuihukumu dhambi katika mwili ili kwamba ajitwalie yeye mwenyewe kanisa tukufu, lililokombolewa, ambalo litaamini tu Neno la Mungu na siyo kulikana, kama Hawa alivyofanya, kwa maarifa ya uelewa wa wanadamu (Mwanzo 3:1-7). Unaliona hilo?.

Hilo ndilo wazo la Kristo. Ndilo wazo la Mungu. Kule kuzaliwa kwa pili kunalifunua hilo. Na kama mtu anasema amezaliwa mara ya pili na kujaribu kuziweka hizo ahadi za kristo katika siku hizi za mwisho kwa wakati mwingine, kumfanya yeye Kristo Jana, lakini siyo leo, hapa huyo mtu au Nafsi hiyo imeingizwa kwenye udanganyifu na shetani. Na kama huyo mtu anasema anaamini hilo, na haidhihiriki yenyewe kupitia kwake

Yesu alisema katika Marko 16:17-18, ishara hizi zitafuatana na hao waaminiokatika ulimwengu wote na katika kila wakati kutoa nje mashetani, na kusema kwa lugha, na madhihirisho hayo yote makuu ya karama ambayo yatafuata, kwamba wata – siyo kwamba pengine, wanapaswa kufanya hayo. Na Mbingu na nchi zitapita lakini Neno lake halitapita kamwe (Matayo 24:35).

Kwa hiyo ni Kristo mwenyewe akijifunua ndani ya mtu iwe anatomia ufahamu wa kiakili au pengine hata hajui ABC. Nusu ya Mitume hawakuzijua. Hiyo ni kweli lakini walimjua Kristo [6].

Kumjua yeye ni uzima, ile nafsi, Kristo mwenyewe, siyo kulinganisha ni ufunuo ambao Mungu mwenyewe anajenga kanisa lake. Na kama hatujengi katika kanisa lile lile Biblia ilisema. “Habibi, kwa Imani” Na Imani ni ufunuo wa kiungu, Unaona? Imani ni ufunuo wa

Kiungu. Sawa hasa. Jambo hili lote limejengwa juu ya ufunuo na ni mpaka tu hili lifunuliwe kwako..... yesu alisema, nakushukuru Baba, kwamba mambo haya umewaficha wenye hekima wa dunia, ukawafunulia watoto wachanga waweza kujifunza (Matayo 11:25). Unaona? Jambo lote limejengwa pale; lazima umjue utu wake [7].

Siyo kujua Neno lake ambalo kunakupa wewe – kulijua hilo, haikupi uzima wa milele. Kumjua Yeye, Biblia ilisema.... Kumjua yeye ni uzima wa milele’ siyo kujua Neno lake, kumjua yeye (Yohana 17:8). [8].

Hawakuwatambua kamwe Petro na Yohana, kwamba walikuwa wametoka kwenye seminary Fulani walisema walitambua na kujua kwamba walikuwa pamoja na Kristo walipomponya kiwete yule pale mlangoni. Walijua walikuwa pamoja na Kristo (Yesu) (Matendo 4:13-22).

Kuzaliwa mara ya pili ni Kristo, ni ufunuo. Mungu amefunua kwako siri hii kuu, na hiyo ndiyo kuzaliwa kwa pili (1Petro 1:22-23). Sasa, utafanyaje hilo kundi lote utakapolikuta hilo kundi lote mahali pamoja, ambapo ufunuo wote uko ni mkamilifu na unakubaliana, na Mungu akilieleleza kupitia Neno lake kwa matendo yale yale, mambo yale yale aliyoyatenda, alilifanya Neno lidhihirike? Kama tu kanisa lingejua nafasi yake. Na siku moja litajua. Hapo unyakuo utafanyika litakapojua lenyewe ni nani.

Sasa, angalia unasema, Ndugu Branham, lakini hiyo siyo..... oh, ndiyo, iko hivyo, pia, ni kweli.

Je uliona hilo? Paulo hakumfahamu Yesu kimwili. Paulo hakumfahamu. Njia pekee ambayo Paulo alimjua Yeye ilikuwa ni kwa ufunuo, kwa maono, hiyo ni kweli? (Wagalatia 1:11-20) Paulo alimfahamu Yesu kwa njia ya ufunuo, kama Petro alivyomfahamu.

Petro alimwona Yeye kwa Jinsi ya mwili, lakini hakumfahamu kwa jinsi ya mwili, kwa sababu Yesu alisema hivyo. Mwili na damu havikukufunulia hili. Hata maisha yangu mwenyewe hayakukufunulia hili, bali ni Baba yangu aliyeminguni amekufunulia jambo hilo” kwamba Yeye ni Neno la Mungu. “Na juu ya mwamba huu nitalijenga Kanisa”. Petro hakumjua Yeye kwa jinsi ya mwili.

Watu walitembea na kumshika na kila kitu kile. Paulo alikuwa na kitu kikubwa kuliko yoyote miongoni mwa mitume walivyokuwa navyo. Unaona? Walisema, vema nina ufunuo zaidi ya wewe Paulo, kwa sababu unajua, nilitembea naye. Nilienda kuvua naye siku moja, nilimsikia akizungumza. Aliketi mtubwini pamoja nami na baada ya kuniambia mimi. Twende hapa na tuvua samaki mahali pale, na tutapata samaki zaidi. Na tukafanya hivyo. Unaona, tulimwona akifanya mambo”.

Lakini Paulo alimwona Yeye baada ya kufa kwake, kuzikwa, kufufuka tena, na akijidhihirisha Mwenyewe katika nguzo ya moto ambayo iliwaongoza wana wa Israeli, akijua..... Paulo, akiwa ni Myahudi, hangeweza kamwe aite hiyo Bwana isipokuwa aliona udhihirisho wa kwamba alikuwa nyuma kule Yule, jana, leo na hata milele. Alisema Paulo....kwa maneno mengine, mimi ni Mungu yule yule leo ambaye nilikuwepo jana. Na Hapa niko katika Nuru ile ile nguzo ya moto ambayo Musa alizungumza nayo katika kijiti kilichokuwa kinawaka moto’. Sio ajabu aliweza kutenganisha sheria na Neema hapa katika kitabu cha Waebrania.

Alikutana na nguzo ile ile ya moto. Alisema. Mimi ni Yesu, unayemuudhi”. (Matendo 9:1-20).

Paulo alimjua Yeye kwa ufunuo tu. Petro alimjua kwa ufunuo. Alitembea naye, alizungumza naye, kwa hiyo, unaweza ukaliweka hili Neno.... Sasa, nimesema hilo tu, Yeye alikuwa ni Neno. Sasa, Mtheolojia (msomi) anaweza akakaa chini na kusoma hilo. Neno mpaka aweze kuifunga akili yako kwa upande wowote, kama angehitaji kufanya hivyo kwa sababu ana akili, mjanja. Mchukue Kuhani wa Kikatoliki, au siyo hasa wa aina hiyo ambaye amefundishwa theolojia vizuri katika Biblia, Ndugu wa Kibaptisti au aina hiyo; atakufanya uwazie kwamba hujui kitu unaona? Inapokuja kwenye kuzungumza.... Kwa nini? Unaona? Kwa sababu amemjua yeye kwa jinsi ya mwili, lile Neno.

Lakini njia pekee uwezayo kuokolewa ni kumjua kwa ufunuo. Kama naweza kuchukua... naweza chukua mafundisho ya Kipresbateria na kuwafunga ninyi Wapentekoste mpaka hamwezi kujua.... Naweza kuchukua mafundisho ya kibaptisti na kuwaonyesha ninyi wapentekoste vitu milioni msivyovijua, hata hivyo ni kweli. Lakini hilo silo hilo. Hilo siyo kanisa lake, hilo silo kanisa lake. Kanisa lake ni Yeye mwenyewe akifunuliwa (Amen. Unaona hilo?) na akielelezwa na Neno kwamba Yeye ni Mungu.

Wawezaje kusema, “Baba, mwana na Roho Mtakatifu tena ubatizwe hivyo? Upagani. Kweli, wawezaje kusema unamjua Yesu Kristo Kwamba yeye ni Neno, wakati hakuna andiko katika Biblia, hakuna mahali ambapo mtu yeyote amebatizwa kwa jina la Baba na mwana na Roho Mtakatifu?

Na ninyi watu wa Yesu pekee, mnatumia jina la Yesu kwa kubatizia, mimi binafsi nawajua wanne au watano ninaofahamiana nao. Sasa unaona kule madhehebu yanakowaongoza kwake? Hilo ndilo Giza, udhihirisho wa Kaini, aliyeleta matunda badala ya Damu. Lakini ufunuo unakuja kupitia Damu, kupitia Yesu Kristo, ambaye ni Damu ya Mungu damu iliyombwa katika tumbo la Mariamu.

Na Paulo alimjua Yeye kwa ufunuo. Hivyo ndivyo tunavyo mjua leo, na ni njia pekee uwezayo kumjua yeye. Siyo kusema, mimi ni Mmethodist”. Hiyo haimaanishi kitu.’ Mimi ni Mbaptist” hiyo haimaanishi kitu” “Mimi ni Mkatoliki”. Hiyo haimaanishi kitu. Lakini kwa ufunuo kwamba Mungu amefunua Neno Kwako. Yeye ni Neno, na Utajuaje kuwa Neno limefunuliwa, linaishi lenyewe na kujieleleza lenyewe kupitia wewe oh.

Makanisa yamesahau kwa muda mrefu ule ufunuo mkuu. Hiyo ni kweli. Ufunuo wa kweli, wameusahau huo. Wamekubali ujumbe wa kiakili, uanachama, maarifa badala ya ufunuo wa kweli wa Neno.

Ni Yesu Kristo, kuzaliwa mara ya pili ufunuo ndani yako kwamba amechukua nafasi ya kwanza, ili aweze kulidhihirisha Neno lake. Na kitu chochote alichohidi siku za mwisho, atakifanya kitimie kupitia mwili wake kadri anavyo tenda kazi. Amina. Ni hasa Neno la Mungu likifanywa dhahiri.

Angalia ni vizuri, sawa kama ilivyokuwa siku za Kristo... Mungu anao ufunuo huo wa ufunuo wa Yesu Kristo akiushikilia yeye mwenyewe. Unaamini hilo? Shule za theolojia haziwezi hata kidogo kuona. Yesu alisema hivyo (kama unataka kusoma hilo sasa) katika Mt. Matayo 11:25 na 27 "Nakushukuru wewe, oo Baba Baba Mungu wa mbingu na nchi, kwamba umeyaficha haya machoni pa wenye hekima na akili, na ukawafunulia watoto wachanga waliotayari kujifunza"

Kwa hiyo sasa, hakuna shule, hakuna mtheolojia, wala mafundisho ya Biblia, yaliyo katika shule yoyote ambayo yanajua chochote juu ya hilo. Hawawezi kujua lolote juu ya hilo. Haiwezekani kwao kujua chochote juu ya hilo. Mungu amezificha hisi za kujua hilo hata kwa walimu walio wateule na vitu vyote pia. Ni kitu cha kibinafsi, jambo la mtu mmoja yule ambaye Kristo amejifunua kwake. Na kama unasema, "Yeye amefunuliwa kwangu," ', na kama maisha yale Kristo aliyoyafanya katika Biblia (maisha yale yaliyokuwa ndani yake) hayaonekani yakidhihirika ndani yako, hapo sasa ufunuo wako siyo sahihi.

Kama nikiweka maisha ya m'boga katika uhai wa mti wa mpeasi, utazaa maboga. Kwa matunda yao mtawatambua " (Matayo 7:16-20). Hiyo ni kweli kabisa. Na kama mwanzo uliweka mti (mzabibu) na ukazaa vichala vya zabibu (chipukizi la kwanza kutokea litazaa zabibu), lingine likazaa malimao, lingine likazaa mapeasi, na lingine likazaa maepo, lazima kuna matawi yaliyopandikizwa katika huo mzabibu, ambayo yanazaa maisha yao wenyewe (Yohana 15:1-7).

Kila dhehebu litazaa matunda yake mwenyewe. Lakini kama mzabibu ule wa asili utatoa chipukizi lingine, litazaa zabibu kama lile la kwanza lilivyofanya. Na kama maisha ya Yesu Kristo yatatoa (kundi) mwili mwingine wa waamini, litazaa matunda yale yale ambayo wale wa kwanza walizaa; wataandika kitabu cha matendo nyuma yake, kwa sababu itakuwa ni maisha yale yale. Unaona, ninachomaanisha? Huwezi ukawa mbali na hilo ni yale maisha ya Kristo ndani yako Yakiwa yameingizwa ndani yako kwa Roho Mtakatifu mwenyewe, akiishi maisha kupitia wewe.

Angalia, Mungu anashikilia huu ufunuo peke yake. Hakuna Mtheolojia anayeweza kukuambia. Haujulikani, umefichwa kwao hawajui lolote kuhusu huo. Hata shuleni pia ..." vema" unasema mimi nina Ph. LL.D. Unafanya

tu... Kwangu mimi na nina mwamini Mungu na kwa mwamini yoyote halisi, wa kweli, hiyo inamaanisha uko umbali huo; umejaribu kwenda mbali. Mungu hajulikani kwa Elimu, hajulikani kwa jinsi ya kuweza kumuelezea.

Mungu anajulikana kwa urahisi na kwa ufunuo wa Yesu Kristo kwa mtu yule asiyejua kabisa kusoma. Unaona? Sio theolojia yako; ni ufunuo wa Yesu Kristo. " juu ya mwamba huu, nitalijenga kanisa langu." Hakuna mwamba mwingine unaokubaliwa: hakuna kitu chochote kinachokubalika, hakuna jiwe lingine la warumi; hakuna mwamba mwingine wa Kiprotestanti, sio shule nyingine, hapana na shule nyingine. Hakuna na hakuna kitu chochote. Lakini ni hasa kwa ufunuo wa Yesu Kristo katika kule kuzaliwa upya. Yeye amezaliwa pale na anaingiza uhai wake mwenyewe na uhai wako umeondoka wakolosai 3:1-4 na uhai wake mwenyewe unajitokeza wenyewe kupitia wewe pamoja na kuchukua nafasi ya kwanza miongoni mwa watu (wakolosai 1:18) kwamba wanaona maisha yaleyale na kazi, na ishara na miujiza kwamba alifanya na anafanya jambo lilile kupitia wewe. Nje ya hapo, na yote yaliyobakia wala hayatajwi kabisa.

Angalia ufunuo mkuu wa Mungu ukijifunua. Kwa kukosa ufunuo huo ndio maana tuna migawanyiko mingi sana kati yetu na vitu vingi vya dhahira, migawanyiko mingi miongoni mwetu ni kwa sababu watu hawana huu ufunuo unaona, wanakosa huu ufunuo: Waalimu [9].

Watoto wasiotii ina maana.... "kutokutii" ina maana ya "uasi" nililiangalia hilo katika dikishenari ili kuwa na uhakika. Uasi, uasi dhidi ya nini? Neno la Mungu lililofunuliwa. Kama Kaini aliasi dhidi ya ufunuo aliofunuliwa Habili, ukithibitishwa na Mungu kwamba ni Haki.... na Kaini akaasi dhidi yake na kumuua ndugu yake. Mafarisayo wakiwa na maarifa yao ya kidhehebu juu ya Neno la Mungu lilivyokuwa, walichagua watu wasiofaa, wakaasi dhidi ya Neno la Mungu lililodhihirishwa na kuthibitishwa katika siku yao, Yesu Kristo na kumuua Yeye. Hiyo ni kweli? Hivyo ndiyo wana

wa uasi walivyo, wanaasi dhiki ya Neno la Mungu. Sasa unaona pale walipo? "oh siku za miujiza zimepita. Yesu Kristo sio yule yule hakuna kitu kama ubatizo wa Roho Mtakatifu. Mambo hayo yote ni upumbavu. Uasi, hawahitaji waseme mambo mawili, waseme moja tu. Hilo tu; huo ni uasi hapo hapo. Hawawezi kusema, "Huna macho wewe; wewe huna masikio" (Ikor 12:16-20). Unapaswa kuchukua mwili wote, Neno lote [10].

Lakini sasa, Mungu alisema katika siku za mwisho atachukuwa watu waliooshwa kwa damu yake. Na kwamba aliwajua kimbele kwamba watakuwa pale; lazima wawe pale. Mungu amesema hivyo. Na itafunua.... na ishara ile kwamba mimi ni--Malaki 4:5-6, na vile ambavyo angefanya - kurudisha tena, kuyaleta tena mambo yake makuu ya siku za mwisho ambayo aliyaahidi. Kwamba Angeleta ufunuo. Atafanya nini? Malaki 4 italeta tena imani ya mababa kwa watoto. Unaona? Hiyo ni kweli kuleta jambo lilile, Nguzo ya moto ile ile inakuja na

kuonekana, ishara zile zile, miujiza ile ile, Yesu yule yule, ikimfanya Yeye yule, akihubiriwa vile vile, akithibitishwa kuwa ni Yule jana leo na hata milele.

Charles E. Y. Kanju,
Box 553 Korogwe - Tanga
E-mail: Chaelika@livel.com
Cellphone: 0784 704299/ 0718230098

“ Lakini nitawarudishia tena”, asema Bwana, “miaka yote” (Joel 2:25-27). Nini?—“Miujiza yote na maajabu walioiacha,” nitawarudisha tena kule mwanzo kwenye ule mti wa asili tena, na nitawarudishia, asema Bwana. Nabii huyo alikuwa nabii aliyethibitishwa. Maneno yake ilibidi yatimie. Amen.

Roho Mtakatifu pekee ndiye mfunuaji wa Neno la ufunuo la Kristo na amekuwapo katika nyakati zote. Kumbuka... Nyakati zote? Neno la Mungu lilikuja kwa nani? Manabii pekee. Hiyo ni kweli, Je ni kweli? Nabii inapasa athibitishwe kwanza. Siyo kwa sababu amesema yeye ni Nabii, kwa sababu amezaliwa akiwa ni Nabii na akahakikishwa kuwa ni Nabii, na kila alichosema kilikuwa hasa ni Neno. Na kikatukia hapo, sasa kitu kingine chochote cha tofauti, kiachilie kupite. unaona? Ilikuwa Neno la Bwana lilikuja tu kwa Roho Mtakatifu. Biblia ilisema, “Watu wa zamani, walivuviwa na Roho Mtakatifu kuandika Neno” (2Petro 1:20-21) [11].

Unakumbuka katika Danieli 12:9-10 alisema “Wenye hekima wataelewa katika siku za mwisho”. Yeye amepewa hilo.

Roho wa hekima anakuja katika kanisa, kufanya kanisa lielewe na ufunuo wa Roho Mtakatifu – akilileta kanisa na kuliingiza ndani na kufunua ni siku gani tunayoishi ndani yake (waefeso 1:15-23). Sawa sawa kama vile Gabriel alivyomjilia Daniel (Daniel 10/12), Roho Mtakatifu anakuja kanisani katika siku za mwisho kufunua mambo haya makuu, ya kindani, mambo ya siri. Mnaelewa sasa ? [12].

Nukuu za Kiingereza

[1] Nyakati saba za kanisa uk 124,83

[2] Lile shitaka Vol. 2 na 19 uk. 43;

[3] waamini wa aina tatu uk.9 [4] Kristo ni siri ya Mungu iliyofunuliwa (kitabu. 3 no7)[5] Kiu-uk.43 Aya 150-151

[6] Kristo ni siri ya Mungu iliyofunuliwa uk. 36-37

[7] Kiu uk. 18 [8] mabwana tunataka kumwona Yesu uk. 22

[9] Kristo ni siri ya Mungu iliyofunuliwa uk. 37-40,43-45

[10] Mungu wa wakati huu mwovu (kitabu. 4 na. 9) uk. 168.

[11] Kristo ni siri ya Mungu iliyofunuliwa uk. 49.

[12] Majuma sabini ya Daniel Aya 68

Jiwe la kiroho la kujengea na 148 kutoka Neno lililofunuliwa la saa hii, iliyokusaywa na Gerd Rodewald, Friedenstr. 69, D-75328 Schomberg Germany, simu (+49) 72357613 Fax – 3306

Atakuja mmoja na ujumbe ambao ni moja kwa moja ni Biblia na kazi ya haraka itaizunguka dunia zile mbegu zitaingizwa katika magazeti na vitu vya kusomea, mpaka kila mbegu ya Mungu iliyoteuliwa kimbele imesikia hilo ndugu Branham katika mwenendo utaratibu na mafundisho uk 724.

Kwa nakala zaidi andika kwa